**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KIZAGA – IRAMBA MKOA WA SINGIDA

**OFISI YA WAZIRI MKUU,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI KIZAGA**

S.L.P 12 KIOMBOI-IRAMBA,
SINGIDA.

Tarehe………………………

MKUU WA SHULE: JUDITH A. MWASAMBAPA
SIMU: **0713834401/0755198903**
Barua pepe: kizagasec2024@gmail.com.
MAKAMU MKUU WA SHULE: **0759150910**

NDG, MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI:
……………………………………………………………………………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIZAGA, HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA MKOA WA SINGIDA

1. **UTANGULIZI**
   Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari KIZAGA iliyopo Wilaya ya Iramba katika Mkoa wa Singida mwaka…………… Shule ya sekondari Kizaga, ni shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, na ni shule ya bweni (wasichana) kwa kidato cha tano na sita. Tahasusi zilizopo shuleni ni CBG na HKL. **KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIZAGA**.
2. **MAHALI SHULE ILIPO**
   Shule ipo umbali wa mita **300** kutoka barabara kuu inayotoka Singida kwenda mwanza. Kwa wanaosafiri kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mikoa ya Kaskazini, Nyanda za juu kusini, Dar es salaam, Kanda ya kati, watashukia mji wa Misigiri.

   Nauli kutoka Misigiri hadi Kizaga sekondari ni Tshs. 2,000 kwa usafilri wa Bajaji.

   Shule itafunguliwa tarehe kama **itakavyoelekezwa na serikali kupitia vyombo vya habari**, unatakiwa kufika shuleni tarehe hiyo bila kukosa. Aidha una muda mrefu wa kumuandaa mtoto hakuna sababu ya kuchelewa kuripoti shule! Ninasisitiza mwanafunzi afike shuleni mapema tarehe husika muda

wa kuripoti ni kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na moja na nusu jioni. Kama kuna dharura tumia namba za shule kuutarifu uongozi.

## 3. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

### 3.1: MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Shule ni ya mchepuo wa sayansi na Sanaa. Tahasusi zilizopo kwa sasa ni CBG na HKL. Masomo yanayofundishwa ni pamoja na Chemistry, Biology, Geography, Kiswahili, English language, Historia ya Tanzania na maadili, Academic communication na Basic Applied Mathematics

### 3.2: SARE YA SHULE

a) Sare ya shule [Darasani] ni **sketi mbili ambazo zitashonewa shuleni ili kundoa mkanganyiko wa rangi na mashono kwa gharama ya tshs 35,000/- Kwa kila sketi moja.**
b) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
c) Wanafunzi wanaovaa hijabu (juba) iwe usawa wa mikono, kitambaa cheupe aina ya halua (kisiwe aina nyingine).
d) Viatu vya shule vyeusi vya Ngozi (kisigino kifupi) jozi mbili, soksi nyeupe ndefu jozi mbli.
e) **Sare ya michezo** kila mwanafunzi aje na raba jozi moja nyeusi, **track suit ya kijani**, jezi nyeusi (bukta na tshirt), soksi ndefu nyeusi za michezo
f) Aje na Sweta rangi nyeusi lenye shape ya V mbele,
g) Aje na nguo za kushindia (**shamba dress)** gauni lenye kitambaa kizito rangi ya kijani kibichi (kijani jeshi) aina ya mshono upo mwisho mwa fomu hii. **Wanaovaa hijabu washone hijabu ya kushindia rangi ya kijani kibichi.**
h) **Tisheti mbili rangi ya kijivu nyeupe** itavaliwa siku ya Ijumaa.
i) Aidha mwanafunzi anaweza kuja pull neck (kaba shingo) **NYEUPE**.

**NB. Nguo za nyumbani/viatu ambavyo si vya shule haviruhusiwi kabisa. Anapokuja kuripoti atatumia track suit.**

## 4. MICHANGO MUHIMU YA SHULE

### 4.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:

i. Madaftari makubwa (counter book quire 4 kulingana na idadi ya masomo yako) madaftari nane na madaftari madogo 8 kwa ajili ya majaribio ya ndani.
ii. **Ream (A4) Mbili** (2) aina ya (double A 80gsm) kwa ajili ya shughuli za Kitaaluma.

iii. Dissection Kit **ILIYOKAMILIKA** na Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma sayansi na Stop watch moja.
iv. Jalada au file jipya aina ya (Spring file) moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu na maendeleo yake kitaaluma hapa shuleni.
v. Uje na vitabu vinavyoendana na tahasusi yako
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

### 4.2: MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI, MALAZI NA CHAKULA

(a) Jembe moja lenye mpini kwa michepuo yote
(b) Squeezer (1) kwa mchepuo wa CBG
(c) Mfagio (1) wa sakafu (soft broom) kwa michepuo yote
(d) Sabuni ya kusafishia chooni (Lita 5) kwa michepuo yote
(e) Fyekeo (kwanja) lililonolewa (1) kwa michepuo yote
(f) Hard broom (1) kwa mchepuo wa HKL
(g) Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) lenye mfuniko na dumu la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa – kila mmoja
(h) Mashuka Jozi 2 rangi ya pink na foronya zake, blanket 1, godoro 1 (inch2.5x6), chandarua 1 (*nyeupe pembe nne) kwa size ya godoro lake.*
(i) Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha
(j) Aje na taulo ndefu, kandambili, kanga/vitenge jozi moja tu, atatumia wakati wa kuoga.
(k) Pajama la kulalia

NB: Kwa wanafunzi wasioweza kusafiri na mizigo kama vile MAGODORO, YANAPATIKANA MADUKANI JIRANI NA SHULE KWA TSH.50,000/=, TRUCK SUTI (Kwa shilingi 25,000/=).

(l) **Kila mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA**; kama hana bima mwanafunzi aje na Tshs **50,400/=** kwa ajili ya Bima kubwa. Aje na fedha atakatiwa shuleni.

### 5. MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia **Tsh. 80,000/=** kwa ajili ya uendeshaji wa shule. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **50601200048 – Kizaga Secondary school Recurrent A/C – NMB –** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip) aje nayo anaporipoti shule.

## 6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 6.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Uvumilivu kwa wanafunzi wenzake, walimu na watumishi wasio walimu na kuwa na utii kwa watu wote.
xii. Kila mwanafunzi anapaswa kutii wito wa dharura , kwa kuhudhuria mahali alipoitwa
xiii. Mwanafunzi awapo shuleni, azingatie matumizi sahahi ya sare za shule.
xiv. Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za kidini kiutamaduni na kisiasa zilizomo katika jumuiya yetu.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni au kifaa chochote kinachotumia umeme wala haruhusiwi kuhifadhi kifaa hicho kwa mtumishi yeyote hapa shuleni.**

**6.2: Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali za shule, mali za watumishi, za jamii na mali za wanafunzi wengine;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo na au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

    NB: Kizaga Sekondari wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi vii. Kufuga ndevu;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara, kama vile cocaine, mirungi na aina nyinginezo. x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kusababisha mimba;
xi. Makossa mengine ya jinai;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule bila ruhusa.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, Wimbo wa Taifa, Nembo ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xvii. Kukataa adhabu yeyote **halali kwa makusudi**
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB:**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA MWANZO WA MAELEKEZO HAYA.**

JUDITH A. MWASAMBAPA
MKUU WA SHULE

KARIBU SANA KIZAGA SEKONDARI

FOMU A:

Picha
Ya
mwanafunzi

OFISI YA WAZIRI MKUUTAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

SHULE YA SEKONDARI KIZAGA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA MWANAFUNZI

**A: TAARIFA ZA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

i.Jina kamili…………………………………………………………………….

ii.Tarehe ya kuzaliwa…………………..Wilaya………………MKOA………..

iii Dini……………………….Dhehebu………………………………………….

Mahali atakapokuwa anaenda wakati wa likzo:

i.Jina…………………………Uhusianao……………..Mahali……………..

ii.Jina…………………………Uhusiano………………Mahali……………..

Kukubali nafasi:

Mimi……………………………………nimesoma maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Kizaga. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutii sheria za shule. Nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na kuchapa kazi za mikono kwa bidii, kutunza mazingira, kushiriki kikamilifu ratiba yote ya shule ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake NA NINAAHIDI KUWA MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU.

Saini………………………..Tarehe……………………………………………………….

B: TAARIFA ZA MZAZI

| Picha<br>Ya<br>Mzazi/mlezi |
|---|

i. Jina kamili…………………………………………………………

ii. Yeye ni mzazi …………….(NDIYO) au mlezi……………….(HAPANA)

iii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi……………………………………….

iv. Kazi yake……………………………………………………………

v. Anwani ya kazini……………………………………………………

vi. Namba ya simu……………………………………………………….

vii. Anwani ya nyumbani…………………………………………………………

viii. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:

Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wanagu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondari Kizaga.

Jina……………………………………..Saini……………………Tarehe……………

**FORM B:**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**:

TO: The Medical Officer

________________________

________________________

________________________

FROM: The Headmistress
Kizaga Secondary School
P.O.BOX 12 Kiomboi-Iramba
SINGIDA




NAME OF THE STUDENT________________________________

Please examine the above named Student as to her fitness for joining our Secondary School year 2026/2027

Signature ________________________

**PART B**:

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by Medical Officer)**

I have examined the above named person and discovered that she is__________

____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________

Date_____________________ Signature _________________________

Station___________________ Designation __


SHULE YA

SEKONDARI KIZAGA

S. L. P 12 KIOMBOI-

IRAMBA SINGIDA.

***MFANO WA MSHONO WA SHAMBA DRESS (Rangi ya kijani kibichi***)





**Draft iwe ya vyumba vikubwa kama inavyoonekana kwenye picha hii.**